Powered By: www.manyamfranchise.com

## 3.2 KISWAHILI (102)

### 3.2.1 Utangulizi

Matokeo ya mtihani wa Kiswahili yamekuwa yakiyumba mwaka baada ya mwingine tangu kuanzishwa kwa mtaala mpya.Watahini wamekuwa wakishuhudia kushuka kwa viwango vya majibu yanayotolewa na watahiniwa .Kadhalika, kumekuwa na kushuka na kupanda kwa asilimia ya watahiniwa wanaotuzwa gredi za juu. Uchanganuzi huu unanuiwa kutathmini utendaji wa watahiniwa katika karatasi mahususi, na katika somo la Kiswahili kwa jumla. Jedwali lifuatalo linaonyesha matokeo ya mtihani wa somo la Kiswahili katika kipindi cha miaka minne (2010 hadi 2013).

***Jedwali 9: Matokeo ya mtihani wa Kiswahili (2010 – 2013)***

| Mwaka | Karatasi | Watahiniwa | Upeo | Alama ya Wastani | Alama Tenganishi |
|---|---|---|---|---|---|
| **2010** | **1** | **354,738** | **40** | **14.32** | **6.53** |
| | **2** | | **80** | **33.77** | **11.96** |
| | **3** | | **80** | **39.22** | **14.09** |
| | | | **200** | **87.10** | **28.73** |
| **2011** | **1** | **410,807** | **40** | **16.43** | **5.61** |
| | **2** | | **80** | **43.45** | **13.18** |
| | **3** | | **80** | **37.76** | **14.96** |
| | **Jumla** | | **200** | **97.63** | **29.81** |
| **2012** | **1** | **433,886** | **40** | **10.43** | **3.63** |
| | **2** | | **80** | **29.06** | **10.77** |
| | **3** | | **80** | **32.14** | **15.15** |
| | **Jumla** | | **200** | **71.62** | **25.71** |
| **2013** | **1** | **445555** | **40** | **18.46** | **5.44** |
| | **2** | | **80** | **29.92** | **12.68** |
| | **3** | | **80** | **34.82** | **14.92** |
| | **Jumla** | | **200** | **83.19** | **29.77** |

Kutokana na jedwali hili, pamoja na takwimu na ripoti nyingine za uchanganuzi wa karatasi za mitihani ya Kiswahili ya mwaka huu, imedhihirika kwamba kwa jumla:

(i) Alama ya wastani ya karatasi ya kwanza (102/1) ya mwaka wa 2013 imepanda kutoka **10.43** mwaka **2012** hadi **18.46** mwaka huu.

(ii) Alama ya juu zaidi iliyotuzwa katika karatasi hii ni **37** ikilinganishwa na **35** mwaka 2012. Ni watahiniwa **watatu** tu waliopata alama hii.

(iii) Alama iliyotuzwa watahiniwa wengi katika karatasi hii ni **17** ikilinganishwa na **08** ya mwaka 2012. Watahiniwa **33, 029**, ndio waliotuzwa alama **17.**

(iv) Karatasi ya kwanza bado haijawatenga vyema wanafunzi bora na wale hafifu.Hili


Powered By: www.manyamfranchise.com

Powered By: www.manyamfranchise.com

linadhihirishwa na alama tenganisho **(5.44)** ambayo iko chini sana ikilinganishwa na alama ya tenganisho ya kikaida **(15.00).** Hali hii inaweza kusababishwa na watahini kuongozwa na kutawaliwa na mtazamo nafsi wakati wa kuzitathmini insha za watahiniwa na kuishia kuwaweka katika viwango sawa au vinavyokaribiana.

(v) Alama ya wastani ya karatasi ya pili imepanda kidogo kutoka **29.06** mwaka 2012 hadi **29.92** mwaka 2013.

(vi) Alama ya juu zaidi iliyotuzwa ni **74** ikilinganishwa na **70** ya mwaka 2012. Ni mwanafunzi **mmoja** tu aliyetuzwa alama hii.

(vii) Alama iliyotuzwa wanafunzi wengi katika karatasi hii ni **25** ikilinganishwa na **30** ya **2012.** Watahiniwa **13,298** ndio waliotuzwa alama hii.

(viii) Karatasi hii iliweza kuwatenga vyema wanafunzi bora na wale hafifu. Alama tenganisho ni **12.68.**

(ix) Utendaji wa watahiniwa katika karatasi ya pili (102/2) bado ni wa kiwango cha chini. Matokeo ya karatasi hii yamezidi kuyumba tangu mwaka wa 2009 .Alama ya wastani ilishuka kwa takriban alama **kumi(10)** mwaka 2010, ikapanda kwa takriban kiwango hichohicho mwaka 2011, na baadaye kushuka kwa alama **kumi na nne nukta thelathini (14.30** ) mwaka 2012. Mwaka 2013 imepanda kwa kiasi kidogo mno.

(x) Matokeo ya karatasi ya tatu (102/3) ya mwaka wa 2013 yamepanda kidogo kutoka **32.14** mwaka 2012 hadi **34.82** mwaka 2013 .

(xi) Alama ya juu zaidi iliyotuzwa katika karatasi hii ni **79** ikilinganishwa na 80 ya mwaka 2012. Ni watahiniwa **watano** tu walituzwa alama hii.

(xii) Alama iliyotuzwa wanafunzi wengi ni **36** ikilinganishwa na **31** ya mwaka 2013 . Watahiniwa **10,763** ndio waliotuzwa alama **36.**

### 3.2.2 Uchanganuzi wa karatasi mahususi

### 3.2.3 Kiswahili Insha (102/1)

***Jedwali 10: Matokeo ya Karatasi ya kwanza ya miaka 2010– 2013***

| Mwaka | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 |
|---|---|---|---|---|
| Alama ya Wastani | 14.32 | 16.43 | 10.43 | 18.46 |
| Alama ya Tenganisho | 6.53 | 5.61 | 3.63 | 5.44 |

Jedwali hili laonyesha kwamba kwa kipindi cha miaka hii minne, (2010-2013), matokeo ya karatasi ya 102/1 yamekuwa yakiyumba , na kwamba watahiniwa wengi hawajaweza kujipatia alama zaidi ya nusu ya alama zote ambazo zinaweza kutuzwa ambazo ni 40. Katika mwaka wa 2013, matokeo yalipanda kwa alama **8.02.**

Tazama uchanganuzi wa swali la kwanza ambalo ndilo lililokuwa la lazima.



Powered By: www.manyamfranchise.com

Powered By: www.manyamfranchise.com

1 **Lazima**:

**Wewe ni meneja katika kampuni ya Jitihada ambapo pamekuwa na visa vya ukiukaji wa maadili ya kikazi. Waandikie wafanyakazi memo kuwaonya dhidi ya jambo hili.**

Swali hili lilimhitaji mtahiniwa kuandika memo kuhusu ukiukaji wa maadili ya kikazi.Watahiniwa wengi hawakumudu kuzingatia muundo wa nje wa utungo wa aina hii.

Tungo za watahiniwa zilidhihirisha kwamba wengi wamekosa ubunifu.Wengi hawakuweza kujadili hoja zilizotarajiwa, hivyo walishindwa kukuza mada kikamilifu. Ni muhimu kukumbuka kuwa watahiniwa walikosa ubunifu hata katika maswali yale mengine.

Imebainika kwamba wanafunzi wengi hawasomi kwa mapana , hivyo hawadiriki kushughulikia masuala ibuka ipasavyo katika tungo zao.

**Ushauri kwa walimu**

Walimu wawatayarishe wanafunzi wao katika maeneo yote bila ubaguzi, kulingana na mahitaji ya silabasi ya Taasisi ya Elimu.

**Mapendekezo**

(i) Walimu wazidi kuwapa wanafunzi mazoezi zaidi katika uandishi wa kiuamilifu.
(ii) Walimu watumie silabasi za K.I.C.D. na K.N.E.C katika ufundishaji wao.
(iii) Wanafunzi wahimizwe kusoma kwa mapana (magazeti, majarida na vitabu katika nyanja anuwai) ili kujifahamisha kuhusu matukio ya kila siku katika jamii na mazingira yao-kitaifa na pia kimataifa. Hili litapalilia ubunifu wao na kuwawezesha kumudu maswali yanayohusu masuala nyeti/masuala ibuka iwapo yatatahiniwa. Haitoshi kujifunga katika masuala yaliyo vitabuni pekee.
(iv) Wanafunzi wahamasishwe kufasiri maswali kwa uangalifu mkubwa huku wakizingatia maneno muhimu.

### 3.2.4 Kiswahili Lugha (102/2)

***Jedwali 11: Matokeo ya Karatasi ya pili (102/2) ya miaka 2010 hadi 2013***

| Mwaka | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 |
|---|---|---|---|---|
| Alama ya Wastani | 33.77 | 43.45 | 29.06 | 29.92 |
| Alama ya Tenganisho | 14.09 | 13.18 | 10.77 | 12.68 |

Matokeo ya karatasi ya 102/2 yamepanda kidogo mwaka wa 2013 kwa alama.

Swali la **tatu** ndilo lililowatatiza watahiniwa zaidi, ingawa wengi pia walipoteza alama katika swali la ufahamu na ufupisho na isimujamii. Tutachanganua swali la tatu.


Powered By: www.manyamfranchise.com

Powered By: www.manyamfranchise.com

**Swali la 3 : MATUMIZI YA LUGHA**

(a) (i) Eleza maana ya sauti mwambatano. (alama 2)

(ii) Andika sauti mwambatano inayotamkiwa kwenye ufizi. (alama 1)

(b) Andika sentensi ifuatayo upya ukibadilisha neno lililopigiwa mstari kuwa kielezi.

Komu ameshona nguo <u>nzuri</u> na kuiuza sokoni. (alama 1)

(c) Tunga sentensi mojamoja kubainisha: (alama 4)

(i) kihusishi cha wakati

(ii) kivumishi cha pekee chenye maana, "bila kubagua".

(d) Andika sentensi ifuatayo katika hali yakinishi.

Askari wasipopiga doria wala kushirikiana na raia hawatakuwa wametuhakikishia usalama. (alama 2)

(e) Bainisha mofimu katika neno:

atamnywea (alama 3)

(f) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo:

Madebe hayo yatasafirishwa pamoja na nyundo hizi. (alama 2)

(g) Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo:

Ingawa mshahara wake si mkubwa anaikimu familia yake. (alama 2)

(h) Tunga sentensi **tatu** kuonyesha matumizi **matatu** tofauti ya kiambishi 'li'. (alama 3)

(i) (i) Eleza maana ya sentensi ya masharti. (alama 1)

(ii) Tunga sentensi ya masharti. (alama 2)

(j) Tumia kiwakilishi cha 'a' unganifu katika sentensi kuonyesha:

(i) umilikaji (alama 2)

(ii) nafasi katika orodha au nafasi katika kundi (alama 2)

(k) Tunga sentensi yenye kikundi tenzi chenye muundo ufuatao:

Kitenzi kisaidizi, kitenzi kikuu, nomino (alama 2)

(l) Tunga sentensi **mbili** kuonyesha matumizi **mawili** tofauti ya kistari kirefu. (alama 2)


Powered By: www.manyamfranchise.com

Powered By: www.manyamfranchise.com

(m) Unganisha sentensi zifuatazo kuwa sentensi moja bila kurudia kitenzi.

Osore amempigia Ngungui simu. Ngungui amempigia Osore simu. (alama 2)

(n) Andika upya sentensi ifuatayo ukibadilisha vitenzi vilivyomo kuwa nomino:

Mayaka anapotumbuiza huchekesha sana. (alama 2)

(o) Andika maana **tatu** za neno: kanda. (alama 3)

(p) Andika visawe **viwili** vya nahau: enda kombo. (alama 2)

**Maswali katika sehemu hii yalilenga mada mbalimbali za kisarufi kama zilivyopendekezwa na silabasi. Maswali yalimhitaji mtahiniwa kutumia ujuzi wake wa dhana za kisarufi kujibu maswali aliyopewa. Watahiniwa wengi sana walishindwa kumudu dhana za kimsingi za kisarufi kama vile kuandika katika udogo, aina za maneno, na matumizi ya viambishi maalum. Wengine walishindwa kujibu maswali ya kimsingi ya mtamshi bora.Kadhalika ,watahiniwa wengi mno walipoteza alama katika maswali yote, hata ya ufahamu na ufupisho kutokana na makosa ya sarufi na hijai. Wengine hawakumudu kuandika ufupisho ipasavyo. Tazama majibu ya maswali.**

(a) (i) Sauti mwambatano ni sauti mbili au zaidi zinazotamkwa kama sauti moja (k.v. konsonanti na kiyeyusho. Kwa mfano /tw/
**Au**
Sauti moja ambayo ni muungano wa sauti mbili au zaidi. Kwa mfano konsonanti mbili au tatu. Kwa mfano,/nd/ mb/ ngw/

1 x 2 - (Alama 2)

**Au**
Sauti ambayo huundwa kwa konsonanti mbili au tatu zinazotamkwa kama sauti moja, kwa mfano, /ndw/ katika ndwele,ngw/katika jangwa

(ii) mf: / nd/ - katika unda
/ nz/ - katika mwanzo
/ tw/ - katika twalika
/ nw/ - katika shonwa
/zw/ - katika tuzwa
/sw/ - katika naswa
/ndw/ - katika undwa

1x1 - (Alama 1)

Mtahiniwa atumie kielezi cha namna kama ifuatavyo.

(b) Komu ameshona nguo vizuri na kuiuza sokoni
au
Komu aliuza nguo sokoni baada ya kuishona vizuri.

(Alama 2)

(c) (i) Watumie kihusishi cha wakati kama vile, kisha, tangu, halafu, kabla ya, hadi, mpaka, kwa, hata, kufikia, kuanzia. Mfano:
Amekuwa hapa tangu asubuhi.
Aliwasili halafu akaondoka.

(Alama 1)


Powered By: www.manyamfranchise.com

(ii) Watumie mzizi - o - ote pamoja na nomino / viwakilishi katika ngeli mbalimbali.
Kwa mfano: Mwalimu alitaka kumtuma mtoto yeyote.
Nzi hula kitu chochote.
Hakuweza kula tunda lolote. n.k

(d) Askari wakipiga doria na kushirikiana na raia watakuwa wametuhakikishia usalama.
(Alama 2)

(e)

| a | ta | m | nyw | e | a |
|---|---|---|---|---|---|
| - nafsi, **au**<br>- mtenda, **au**<br>- ngeli, **au**<br>- nafsi ya<br>- tatu, **au**<br>umoja **au**<br>- kiima | - wakati ujao | - mtendewa, **au**<br>- nafsi, **au**<br>- nafsi ya tatu mtendewa, **au**<br>-yambwa tendewa, **au**<br>-yambwa kitondo | mzizi | Kauli **au** tendea<br>Kauli **au**<br>- mnyambuliko | - Kiishio, **au**<br>- Kauli tenda |

$6 \times \frac{1}{2}$ (Alama 3)

(f) Videbe hivyo vitasafirishwa pamoja na vijundo hivi.
**au**
Vijidebe hivyo vitasafirishwa pamoja na vijijundo hivi.
2 x 1 - (Alama 2)

(g) (i) Ingawa mshahara wake si mkubwa - tegemezi
(ii) anaikimu familia yake - huru
2 x 1 (Alama 2)

(h) Matumizi ya 'Kiambishi 'li'
(i) Kiambishi cha wakati uliopita - Musa alitutembelea.
(ii) Kiambishi cha ngeli - Tunda liliiva
(iii) Kiambishi cha kauli tendea - Yule alikukimbilia **au** Mtoto amekalia kigoda.
3 x 1 (Alama 3)

(i) (i) Ni sentensi inayoonyesha kutegemeana kwa matendo au hali.
(Alama 1)

(ii) Watumie viambishi na maneno yanayoonyesha kuwa kufanikiwa au kutofanikiwa kwa tukio au tendo moja kunategemea kufanikiwa kwa tukio au tendo lingine. kwa mfano: nge, ngali, ki, kama, iwapo n.k.
(a) Wanafunzi wangefika mapema wangempata mwalimu.
(b) Kotu angalisoma kwa bidii angalifaulu.
(c) Mvua ikinyesha mapema tutapata faida.
(d) Iwapo unataka ufanisi jibidiishe.

**Tanbihi**
Mtahiniwa anaweza kuandika katika hali kanushi kama vile:
(a) Mkulima asingalipanda mapema asingalipata mazao mengi.
(b) Huyu asipojihadhari ataharibikiwa.

Powered By: www.manyamfranchise.com

(c) Iwapo hutaanza safari mapema utachelewa.
(d) Kama utaanza shughuli mapema hutatatizika.
(e) Lazima asome kwa bidii ili afanikiwe

(Alama 2)

(j) (i) La Katunda linapendeza.
**Au**
Tindi anataka cha mwenziwe.

(ii) Atumie viwakilishi vya idadi halisi vinavyotumia a - unganifu. Kwa mfano:
Wa tatu atatuzwa shaba.
**Au**: Mwalimu anamuita wa nne.

1 x 2 - (Alama 2)

(k) Mifano ifuatayo au zaidi inaweza kujitokeza.
Kairu hajawahi kupalilia mtama.
TS T N
**Au**
Huyu ataweza kukupa ufadhili.
TS T N
**Au**
Wanafunzi hawa wangali wanafanya mtihani.
TS T N
**Au**
Musa alikuwa anawafundisha wanawe.
TS T N

1 x 2 - (Alama 2)
alama 2/0

(l) (i) Hutumiwa kutilia mkazo maelezo/kutoa maelezo zaidi/kufafanua au kuonyesha kusisitiza. Kwa mfano:
Alinunua matunda — maembe, machungwa na matango.
(ii) Hutumiwa kuonyesha kubadilika kwa maoni. Kwa mfano:
Waite wale — hapana, hawa.
(iii) Kuonyesha msemaji/usemi halisi, kwa mfano
Utengano ni udhaifu — duma

2 x 1 (Alama 2)

(m) Sentensi ibainishe kauli au hali ya kutendeana. Osore na Ngungui wamepigiana simu.
**Au**
Osore na Ngungui wamepigania simu.

1x2 (Alama 2)

(n) Utumbuizaji wa Mayaka una ucheshi mwingi/sana.
**Au**
Kutumbuiza kwa Mayaka kuna ucheshi mwingi/sana.
**Au**
Kutumbuiza kwa Mayaka kuna kuchekesha kwingi/sana.

1 x 2 - (Alama 2)

(o) Kanda
(i) kutomasa


Powered By: www.manyamfranchise.com

Powered By: www.manyamfranchise.com

(ii) eneo
(iii) aina ya mfuko
(iv) mtu asiyeaminika/laghai/ayari
(v) wingi wa ukanda/mshipi
(vi) malipo kwa mganga
(vii) makasia ya kuogelea
(viii) utepe/mshipi unaotumiwa kunasia sauti/picha
(ix) mtu asiyesimika/hanithi 3 x 1 (Alama 3)

(p) (i) enda mvange
(ii) enda upogo
(iii) enda segemnege
(iv) enda arijojo
(v) enda mrama
(vi) enda benibeni
(vii) enda shoro
(viii) enda tenge 2 x 1 (Alama 2)

**MAPENDEKEZO**

(i) Walimu waendelee kuwapa wanafunzi mazoezi katika vipengele vyote vya kisarufi.
(ii) Wanafunzi wasisitiziwe kwamba baadhi ya maswali ni ya stadi za juu kama matumizi/ utekelezaji na usanisi .Wasitarajie kila mara kupata maswali ya kuchopoa majibu moja kwa moja kutoka kwenye vifungu au kukariri kutoka kumbukumbu zao.
(iii) Wanafunzi wapewe mazoezi ya ufahamu na muhtasari mara kwa mara huku mtiririko ufaao ukisisitizwa ili wapate kuzoea kutumia viunganishi kutiririsha hoja katika kujibu maswali ya muhtasari.
(iv) Walimu wasisitize vipengele vya kimsingi vya sarufi kuanzia kidato cha kwanza hadi kidato cha nne.
(v) Mwelekeo mseto katika ufunzaji uzingatiwe zaidi. Mathalan mwalimu anaweza kutumia fasihi kufunzia mada tata za sarufi, kama vile aina za sentensi. Hili litachangia katika kulihuisha somo la sarufi na kuwafanya wanafunzi kulichangamkia.
(vi) Walimu na wanafunzi watalii maeneo yote ya sajili bila ya kujifunga kwa chache tu ambazo ni za kawaida.
(vii) Masuala yote katika silabasi yafundishwe katika upana wake bila kubagua.

### 3.2.5 Kiswahili Fasihi (102/3)

Matokeo ya karatasi ya tatu (102/3) ya miaka ya 2010 hadi 2013

| Mwaka | 2010 | 2011 | 2012 | 2013 |
|---|---|---|---|---|
| Alama ya Wastani | 39.22 | 37.76 | 32.14 | 34.82 |
| Alama ya Tenganisho | 14.09 | 14.96 | 15.15 | 14.92 |

Matokeo haya yanaonyesha kuwa utendaji wa watahiniwa katika karatasi hii haujafikia kiwango cha kuridhisha.

Tutachanganua swali la kwanza kwani ndilo lililokuwa la lazima.


Powered By: www.manyamfranchise.com

Powered By: www.manyamfranchise.com

## SEHEMU A : FASIHI SIMULIZI

**1 Lazima**

(a) Huku ukitoa mfano, eleza maana ya vitanza ndimi. (alama 2)

(b) Fafanua majukumu **sita** ya vitanza ndimi katika jamii. (alama 6)

(c) Eleza mbinu **sita** unazoweza kutumia katika kukusanya na kuhifadhi habari kuhusu vitanza ndimi. (alama 12)

Swali hili lilimhitaji mtahiniwa :

a) Kutumia ujuzi wake wa vipera vya fasihi simulizi kuchanganua majukumu ya vitanza ndimi.
b) Kutumia ujuzi wake wa mbinu za utafiti wa nyanjani kufafanua mbinu za kutafitia vitanza ndimi.

Hata hivyo, ilidhihirika kwamba asilimia kubwa ya watahiniwa haikumudu kufafanua mbinu za utafiti, pengine kwa kuwa hawakufundishwa.

Kadhalika, watahiniwa wengine walijadili mbinu za kimtindo badala ya mbinu za utafiti.
Pia ilibainika kwamba watahiniwa wengi bado wana mtazamo hasi kuhusu ushairi .Ni watahiniwa wachache tu waliofanya maswali ya ushairi.Watahiniwa hawa hawakupata alama za juu.

1. (a) **Maana ya Vitanza Ndimi**

Vitanza ndimi ni virai/vishazi au sentensi zenye sauti zinazokaribiana au zinazofanana kimatamshi na ambazo hutatiza mtu kuzitamka. Aghalabu huundwa kwa vitate, vitawe, au hata kurudia maneno yale yale katika sentensi. Kwa mfano:

(i) Wali huliwa na mwana wa liwali. Asiyekuwa mwana wa liwali hali wali.
(ii) Wali huliwa na wanawali, wasio wanawali hawali wali.
(iii) Shirika la reli la Rwanda lililiathiri lile la reli la Kenya.
(iv) Mzee aliyevaa koti lililofika gotini alianguka akaumia goti kisha koti lake lenye kufika magotini likachanika. (alama 2)

(b) **Majukumu ya Vitanza ndimi**

(i) Kumzoesha mtoto/mtu kuzitamka sauti au maneno vizuri.
(ii) Ni nyenzo ya burudani. Vikao vya mashindano ya utamkaji hutumiwa kuwachangamsha wanajamii.
(iii) Msingi wa kumsaidia mtoto kujua lugha kwa undani. Huundwa kwa vitate au vitawe, hivyo mtu hujifunza vipengele hivi vya lugha.
(iv) Husaidia kuimarisha uwezo wa kimawasiliano wa anayehusika. Utamkaji wa vitanza ndimi kwa kasi humzoesha mzungumzaji kuweza kuwasilisha hoja bila kusitasita.
(v) Huendeleza utamaduni. Jinsi wanajamii wanavyoshirikishwa katika utamkaji ndivyo wanavyorithishwa utamaduni wao au desturi yenyewe ya kushiriki


Powered By: www.manyamfranchise.com

Powered By: www.manyamfranchise.com

katika utamkaji.

(vi) Hujenga stadi ya ukakamavu. Kadiri mtu anavyoshiriki katika utamkaji ndivyo anavyoimarisha ujasiri wake wa kuzungumza hadharani.

(vii) Huibua ucheshi na kudumisha uhusiano mwema. Utani unaoibuliwa katika mashindano ya utamkaji ni msingi wa kujenga uhusiano.

(viii) Hukuza ubunifu. Wanajamii huweza kubuni vitanza ndimi hapohapo, wakavitamka.

(ix) Ni kitambulisho cha jamii. Kila jamii ina vitanza ndimi vyake vinavyohusu mazingira yake.

(x) Hukuza utangamano katika jamii. Vikao vya mashindano ya utamkaji huwaleta wanajamii pamoja hivyo kujihisi kuwa kundi moja.

(xi) Kuonya/kushauri - baadhi hufumbata maonyo/ushauri. Kwa mfano, Mzaha mzaha huzaa usaha. (6 x 1 = 6)

Kutaja ½ Mfano ½

(c) (i) Utazamaji wa kushiriki au kutoshiriki. Mtu anaweza kushiriki katika kikao cha utamkaji wa vitanza ndimi, hivyo kujua vinavyoendelezwa katika jamii husika.

(ii) Video. Mtu anaweza kupiga picha za video watu wakitamka/wakishindana katika. utamkaji wa vitanza ndimi ili kuja kuchanganua baadaye.

(iii) Matumizi ya hojaji. Mtu anaweza kuandaa maswali katika hojaji ili kudadisi kwa mfano, kama vipo katika jamii fulani, wanaohusika katika vikao vya utamkaji na uundaji wake.

(iv) Kurekodi kimaandishi (kuandika) ili kuvirithisha au hata kuvichanganua baadaye.

(v) Majadiliano ya vikundi lengwa, Mtafiti anaweza kuteua vikundi, kwa mfano, vijana, ili kuchunguza namna wanavyoviunda na kuvitamka, na athari ya vitanza ndimi hivi kwao.

(vi) Mahojiano Mtafiti anaweza kuandaa mahojiano rasmi na kundi / sampuli lengwa ili kuchunguza kwa mfano, majukumu ya vitanza ndimi katika jamii husika

(vii) Matumizi ya vinasa sauti na sidii ili kunasa utamkaji wenyewe na kuchanganua sifa zake.

(viii) Kutumia kumbukumbu ya mtafiti mwenyewe. Utafiti ambaye in mmoja wapo wa wanajamii katika eneo analofanyia utafiti anaweza kurithisha yale anayokumbuka baada ya kuyashuhudia.

(ix) Kusoma majarida na vitabu (maktabani) vyenye habari kuhusu vitanza ndimi.

(6 x 2 = 12)


Powered By: www.manyamfranchise.com

Powered By: www.manyamfranchise.com

### 3.2.6 MAPENDEKEZO

3.2.6.1 Walimu wafundishe vitabu vilivyoteuliwa kwa ukamilifu wake huku wakizingatia vipengele vifuatavyo vya uchanganuzi wa kazi za kifasihi:

a) Dhamira na maudhui
b) Fani , kama vile:
   - Mandhari
   - Ploti
   - Usimulizi
   - Wahusika
   - Muundo
   - Mtindo, kama vile tamathali za usemi, urudiaji, n.k

3.2.6.2 Wanafunzi wahimizwe kutambua masuala muhimu yanayojitokeza katika hadithi zote katika diwani teule ya hadithi fupi.

3.6.2.3 Wanafunzi wawekewe misingi bora katika fasihi simulizi tangu kidato cha kwanza.

3.6.2.4 Walimu wawafundishe wanafunzi wao istilahi muhimu zinazohusiana na ushairi ili kuupalilia ukakamavu wao katika kuyajibu maswali ya ushairi.

### 3.2.7 Uchanganuzi wa mtihani wa Kiswahili kwa jumla.

Uchanganuzi wa mtihani wa mwaka wa 2013 umebainisha kwamba:

3.2.7.1 Alama ya wastani ya somo la Kiswahili imeshuka imepanda **kutoka 71.62** mwaka **2012** hadi **83.19** 2013.

3.2.7.2 Alama wastani ya somo hili imekuwa ikiyumba tangu mwaka wa 2009.

3.2.7.3 Alama ya juu iliyotuzwa katika somo hili ni **177/200.** Ni mwanafunzi **mmoja** tu aliyepata alama hii.

3.2.7.4 Ni asilimia ndogo sana ya watahiniwa iliyopata gredi wasatni **A** na **A-** katika somo hili.

### 3.2.8 Hitimisho

Kutokana na uchanganuzi wa hapo juu, ni dhahiri kwamba matokeo ya somo la Kiswahili bado hayajafikia kiwango cha kuridhisdha.. Ni watahiniwa wachache mno waliofikia viwango vya juu vya utendaji katika karatasi zote tatu.

Ni matumaini yetu kwamba walimu na wanafunzi watafaidi kwa uchanganuzi uliotolewa .Kadhalika tunawahimiza kuyatilia maanani mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti hii ili kuimarisha matokeo ya somo hili..


Powered By: www.manyamfranchise.com